



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS,
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI



TANGAZO

MKURUGENZI WA MANISPAA YA KINONDONI ANAWATANGAZIA WAFUGAJI WOTE KUWA UFUGAJI WA MJINI NI WA NDANI (ZERO GRAZING) NA SI WA KUCHUNGA MIFUGO HIVYO KUZURURISHA MIFUGO NI KOSA CHINI YA SHERIA YA ANIMAL WELFARE ACT 2008 11(1,2) 12, KUCHUNGA MIFUGO MAENEO YA BARABARANI NI KOSA CHINI YA SHERIA YA ANIMAL DISEASE ACT 2003 17 9(1), SHERIA YA PUBLIC HEALTH ACT 2007 52-55

KWA KUWA ZOEZI LA KUKAMATA MIFUGO INAYOZURURA LILIFANYIKA MWEZI MACHI 2022 NA WAFUGAJI WOTE WALIOKUTWA NA KOSA LA KUZURURISHA MIFUGO (MBUZI NA KONDOO) WALILIPA FAINI NA WALIPEWA ILANI NA MASHARTI YA UFUGAJI,

BAADA YA ZOEZI HAKUNA UTEKELEZAJI ULIOFANYIKA NA HIVYO MIFUGO IMEENDELEA KUZURURA BARABARANI NA KUSABISHA KERO KWA WANANCHI IKIWA KUSABABISHA AJALI ZA BARABARANI NA UHARIBIFU WA MAZINGIRA.

KUANZIA TAREHE YA TANGAZO HILI MNYAMA YOYOTE ATAKAEKAMATWA ANAZURURA MMILIKI WA WANYAMA HAO ATACHUKULIWA HATUA KALI ZA KISHERIA IKIWA NI PAMOJA NA KUFIKISHWA MAHAKAMANI.

PIA TANGAZO HILI LINAWATAKA WAFUGAJI WOTE WANAOFUGA MANISPAA YA KINONDONI KUFUATA SHERIA NA TARATIBU ZA UFUGAJI MJINI KWA KUWASILIANA NA MAAFISA MIFUGO WA KATA ILI KUPEWA TARATIBU ZINAZOTAKIWA KWENYE UFUGAJI.

13/6/2022

Hanifa Suleiman Hamza
MKURUGENZI WA MANISPAA



Jiandae kuhesabiwa Siku ya Jumanne tarehe 23 Agosti, 2022